**Adhabu**

Mtu yeyote akikutwa na hatia ya kutenda kosa la hilo Sheria imeainisha adhabu ya kosa hilo kuwa ni ***kifungo kisichopungua miaka ishirini jela.***

### 4.1.4 Ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa kingono

Mtu hatamsababishia mtoto mateso, au aina nyingine ya ukatili, kumpa adhabu zisizo za kibinadamu au kumdhalilisha mtoto ikijumuisha mila na desturi zozote zenye madhara kwa mtoto kimwili au kiakili.

**Adhabu**

Mtu atakayekiuka atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa ***faini isiyopungua milioni moja na isiyozidi shilingi milioni tano au kifungo cha kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili jela*** au ***vyote kwa pamoja.***

### 4.1.5 Kuanzishwa kwa Mabaraza ya watoto

Sheria imeanzisha na kurasimisha mabaraza ya watoto katika ngazi ya kijiji, kata, wilaya, mkoa na ngazi ya taifa ili kuwe na majukwaa yanayowafikia watoto na kujadilian haki zao ,changamoto na zinazowakabili na ustawi wao ili kuweza kuwalinda na matukio ya unyanyasaji na uhalifu katika jamii.

### 4.1.6 Mahakama ya mtoto

Katika kuwezesha utoaji haki kwa watoto kwa wakati na kuboresha ustawi na maslahi ya watoto sharia imeanzisha na kutambua mahakama za watoto kila wilaya kwa ajili ya kusikiliza mashauri ya watoto. Pia sheria imeongeza mahakama ya watoto kuwa na mamlaka ya kushughulikia mashauri ya kuasili watoto ili kuongeza ufanisi na mlundikano wa mashauri katika mahakama nyingine.....

### 4.1.7 Ulinzi wa Mtoto awapo mahabusu

Iwapo mtoto atakuwa amekinzana na sharia na yupo mahabusu sharia inakataza kuchangamana na wahalifu wengine ambao ni watu wazima hata kama ni ndugu. Hii yote ni kumuwekea ulinzi mtoto pale anapokuwa katika mahabusu.

### 4.1.8 Maombi ya kuasili mtoto

Mahakama imeondolewa mamlaka ya kuruhusu mtoto kusafirishwa nje ya nchi wakati wa utoaji wa amri ya mpito kabla ya kukamilika mchakato wa kuasili mtoto kwa lengo la kuhakikisha ulinzi wa mtoto anekusudiwa kuasiliwa kabla ya mahakama kutoa amri.

### 4.1.9 Adhabu na katazo la jumla

Ili kuendelea kuthibiti ulinzi wa mtoto Sheria ya mtoto ***imetoa katazo kwa Mtu yeyote atakayekiuka na kuzalisha, kusambaza, kuuza, kuwashawishi, kuwatishia au kuwaonyesha watoto picha,video au maandishi yenye maudhui ya kingono au ponografia kwa lengo la kuwashawishi kushiriki katika matendo ya kingono atakuwa , anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atalipa faini isiyopungua shilingi laki tano au kifungo cha miezi sita au vyote kwa pamoja na atalipa fidia kwa madhara aliyopata muathiriwa.***

## 5.0 Hitimisho.

Jukumu la ulinzi wa mtoto Ulinzi na usalama wa mtoto ni jukumu la kila mtu na taifa kwa ujumla. Jamii inatakiwa iwe bega kwa bega katika kufanikisha wajibu wa kuhakikisha mtoto analindwa na kuchukua hatua pale ambapo watoto wanaonekana kufanyiwa ukatili.

---


**Kwa maoni, wasiliana na Tume kupitia anuwani ifuatayo:**

Katibu Mtendaji,
Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania,
Jengo la Taaluma Na.1
Barabara ya Mkalama
S.L.P 1718
DODOMA - TANZANIA

tumesheria.tanzania | www.lrct.go.tz
@tumesheria | TumesheriaTv


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



## ULINZI WA MTOTO KATIKA MITANDAO

## ULINZI WA MTOTO KATIKA MITANDAO

### 1. 0 Utangulizi

Tume ya Kurekebisha Tanzania ilianzishwa mwaka 1980 kupitia Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, Sura ya 171. Kwa mujibu wa Sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kupitia na kufanya tafiti za sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na teknolojia.

Tume pia inajukumu la kufanya tathmini za utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kubaini kama malengo ya kutungwa kwa sheria hizo yanafikiwa.

Tume vilevile ina jukumu la kutoa elimu ya sheria kwa umma ili kuweza kuwajengea wananchi uelewa wa sheria mbalimbali na hivyo kusaidia wananchi kushiriki kikamilifu katika maboresho ya sheria.

### 2.1 Mtoto ni nani?

Sheria ya mtoto imetoa tafsiri ya mtoto kuwa mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18.

### 3.1 Ulinzi wa mtoto

Kukua kwa sayansi na teknolojia ni moja ya sababu ya ongezeko la makosa ya ukatili kwa watoto hasa kwa kutumia teknolojia ya kompyuta na mifumo ya tehema. Katika kuhakikisha kwamba mtoto analindwa dhidi ya ukatili, unyanyasaji na udhalilishaji kwa kutumia kompyuta na vifaa vingine vya kielektroniki sheria zilihitaji maboresho ili kuhakikisha mtoto anapewa ulinzi stahiki.

### 4.1 Marekebisho ya sheria (ulinzi wa Mtoto) Namba 6 ya mwaka 2024

Marekebisho hayo yanahusisha sheria ya Makosa ya Mtandao na Sheria ya Mtoto Sura 13 kama ifuatavyo;-

#### 4.1.1 Kutumia kifaa chenye maudhui ya ngono kwa mtoto

**Sheria imekataza mtu yeyote kwa kutumia kompyuta;-**

i. Kuzalisha au kutengeneza kifaa chenye maudhui ya kingono kwa mtoto;

ii. Kupatikana au kutoa kifaa chenye maudhui ya kingono kwa mtoto;

iii. Kusambaza kifaa chenye maudhui ya kingono kwa mtoto;

iv. Kununua kwa matumizi ya mtu binafsi au kwa ajili ya mtu mwingine kifaa chenye maudhui ya kingono kwa mtoto;au

v. Kumlazimisha au kumruhusu mtoto kutumia kifaa chenye maudhui ya kingono kwa mtoto.

**Adhabu**

Mtu yeyote atakayekiuka sheria kwa kufanya makosa hayo atakuwa ametenda kosa la jinai na akitiwa hatiani adhabu yake ni ***faini isiyopungua shilingi milioni hamsini,*** au ataamriwa ***kulipa mara tatu ya faida aliyoipata kwa kutenda kosa hilo*** au ***kifungo kisichopungua miaka saba jela au vyote kwa pamoja.*** Pia mahakama inaweza kutoa amri ya kumlipa fidia mtoto alieathiriwa na makosa hayo.

#### 4.1.2 Ushawishi wa Kutumia Mfumo wa Kompyuta

Sheria imekataza mtu yeyote kushiriki katika kushawishi, kurubuni mtoto kwa kutumia mfumo wa kompyuta, kukutana na mtoto kwa madhumuni ya kushiriki matendo ya ngono kwa;

i. Kulazimisha, kutumia nguvu au vitisho;

ii. Kutumia vibaya mamlaka au nafasi yake;

iii. Kumshawishi mtoto;

iv. Kutumia nafasi ya hali ya mtoto aliye katika mazingira magumu;

v. Kutumia nafasi ya mapungufu ya ugonjwa wa akili kwa mtoto, ulemavu au hali ya utegemezi; au

vi. Kuajiri, kufanya ulaghai, kutumia nguvu kusababisha mtoto kushiriki katika matendo ya ngono kwa kujipatia faida au kufanya unyanyasaji wa aina kama hiyo.

**Adhabu**

Mtu yeyote atakayekiuka sheria kwa kufanya makosa hayo atakuwa ametenda kosa la jinai na akitiwa hatiani adhabu yake ni ***kulipa faini isiyopungua shilingi milioni hamsini***, au ***atalipa mara tatu ya faida aliyoipata kwa kutenda kosa hilo au kifungo kisichopungua miaka saba jela*** au vyote kwa pamoja. Pia mahakama inaweza ***kutoa amri ya kumlipa fidia mtoto alieathiriwa na makosa hayo.***

#### 4.1.3 Ulinzi wa Mtoto dhidi ya Makosa ya Ugaidi Mtandaoni

Ugaidi unahusisha vitendo vya kihalifu mathalani kujeruhi, mauaji, kubomoa miundombinu n.k vinavyofanywa na kikundi cha watu chenye mtazamo wa kuleta hofu katika jamii au kushinikiza serikali au vyombo vya umoja wa mataifa kufanya au kutofanya jambo fulani.

Ili kumlinda mtoto na makosa ya ugaidi katika mtandao sheria imeweka katazo kwa mtu yeyote kwa kutumia mifumo ya kompyuta au tehama kujihusisha, kuwafundisha, kuwashawishi na kuwakusanya watoto kwa lengo la au kufanya ugaidi, atakuwa ametenda kosa.